



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 03 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Waziri wa Afya:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2024/2025.

II. **MASWALI:**

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

11. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Vitendo vya vijana wanaoshika mapanga na kuwanyang'anya wananchi mali zao mchana kweupe na hata usiku, vimeendelea kukithiri katika maeneo mbali mbali nchini.

Je, ni lini Jeshi la Polisi litafanya operesheni maalum ya kutokomeza vitendo hivyo.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

12. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kuna baadhi ya taasisi zinakosa ufanisi kutokana na uhaba wa wafanyakazi wa kada mbali mbali.

Je, ni mkakati gani wa Serikali katika kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

16. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Baadhi ya vituo vya daladala havipo katika hali nzuri ya ujenzi wake na hata uchafu wa mazingira unaozunguka katika maeneo ya vituo hivyo, ikiwa ni pamoja na kituo cha daladala cha Chukwani na Uwanja wa Ndege.

Je, Serekali ina mkakati gani wa kuweka mazingira mazuri katika vituo hivyo.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

67. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi kikubwa vijana wetu wa siku hizi wamekosa maadili mema katika jamii, kwa kuanzia kivazi, tabia na hata wanapozungumza wenyewe na wazee wao.

Ni kwa kiasi gani elimu inayohusiana na maadili inatolewa kwa vijana.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

241. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:
- (a) Kuna vituo vingapi vyta Serikali na watu binafsi vinavyojuhusisha kutoa tiba za wanyama.
 - (b) Tathmini iko vipi juu ya uwepo wa madaktari mahsusini pamoja na ubora wa vifaa tiba vyta wanyama.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

27. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kuitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa juhudi kubwa inazoendelea kuzichukuwa na kuongeza idadi ya ufaulu kwa wanafunzi wa Kidato cha Pili na cha Nne. Hata hivyo, wapo wanafunzi ambao wanashindwa kabisa kuyafikia malengo hayo.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wanafunzi wanaoshindwa kuhitimu kwa kukosa vyeti vyta kumalizia masomo yao.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

98. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Bandari ya Wete ni langoo kuu la kuingizia mizigo na abiria kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba kutoka Unguja, Tanga, na Kenya. Licha ya umuhimu wake kwa maendeleo ya kisiwa cha Pemba, bandari hii inakabiliwa na changamoto nyingi zinazosababisha kupungua kwa ufanisi na ukusanyaji wa mapato.

- (a) Je, ni kiasi gani cha mizigo (tonnes) na idadi ipi ya abiria wanaopita katika bandari hii kila mwaka kati ya 2020 na 2023.
- (b) Je, ni mapato ya kiasi gani bandari hii imeingiza kila mwaka kuanzia mwaka 2020 hadi 2023.

- (c) Kwa muda mrefu Serikali imeahidi kuifanyia matengenezo bandari hii, Je, ni lini bandari hii itatengenezwa na marekebisho gani yanatarajiwa kufanyika ili kuongeza ufanisi wake.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Afya:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
03 Juni, 2024.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA